

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA**



TAARIFA KWA UMMA

Dodoma, 15 Januari, 2025

Wizara ya Afya imepokea tetesi za uwepo wa ugonjwa wa *Marburg* katika Mkoa wa Kagera.

Kufuatia tetesi hizo, Wizara imechukua hatua kadhaa za haraka ikiwemo: kutuma timu ya wataalamu; kufanya uchunguzi wa suala hili; kuchukua sampuli na kufanya vipimo vyaa maabara. Mpaka leo, tarehe 15 Januari 2025, majibu ya uchunguzi wa kimaabara kutoka kwa wahisiwa wote waliochukuliwa sampuli hizo hayajathibisha uwepo wa virusi vyaa Marburg.

Wizara inapenda kuwahakikisha wananchi pamoja na jumuiya ya kimataifa, likiwemo Shirika la Afya Duniani (**World Health Organisation – WHO**), kuwa imeimarisha mifumo ya ufuatiliaji wa magonjwa na itaendelea kutoa taarifa zaidi.

Imetolewa na:

A handwritten signature in black ink, appearing to read "Jenista J. Mhagama (Mb.)".

**Jenista J. Mhagama (Mb).
Waziri wa Afya**